THE KENYA NATIONAL EXAMINATIONS BOARD

PG:04

# STANDARD SEVEN

# KISWAHILI

## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA
## 2021 Muda: Saa 1 dakika 40

**DAY 2**
11:00am -12:40pm

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA (soma maagizo yafuatayo kwa makini.)**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika KARATASI YA MAJIBU na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:
   **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
   **JINA LAKO**
   **JINA LA SHULE YAKO**
5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

**Mfano:**

**Katika kijitabu cha maswali:**

**22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
- A. waraka
- B. barua maalum
- C. barua ya kiofisi
- D. Barua rasmi

Jibu sahihi ni **D**

**Katika karatasi ya majibu:**

2 [A] [B] [C] [D] 12 [A] [B] [C] [D] 22 [A] [B] [C] [D] 32 [A] [B] [C] [D] 42 [A] [B] [C] [D]

Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba 22, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku kimoja tu kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

PRE-GOLD

GEUZA UKURASA

© Stepford Press and Publishers, 2021

**Maswali 1 mpaka 15**

*Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi* 1 *mpaka* 15. *Kwa kila nafasi umepewa majibu manne. Chagua jibu lifaalo* ***zaidi*** *kati ya yale uliyopewa.*

Naam, shukrani zangu za __1__ ziwaendee walimu na wanafunzi wote __2__ kufa kupona kijifunza na __3__ Kiswahili kwa __4__ na mali usiku na mchana. Juhudi __5__ nyingi kama za mchwa wanaojenga kichuguu kwa __6__ zimekiwezesha Kiswahili kupanda na kupanuka kiasi __7__ kufikia ubora unaoaminika na __8__ . Hakika penye nia __9__ njia. Nao umoja ni nguvu __10__ ni udhaifu.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **1.** | A. hati | B. bati | C. chati | D. dhati |
| **2.** | A. wanaojitoa | B. wanaojitolea | C. wanaotoana | D. wanajitoa |
| **3.** | A. kukua | B. kupinga | C. kukuza | D. kukiuka |
| **4.** | A. nguvu | B. pesa | C. haki | D. hali |
| **5.** | A. yao | B. zao | C. lao | D. chao |
| **6.** | A. mawe | B. tope | C. mate | D. mchanga |
| **7.** | A. ya | B. cha | C. kwa | D. la |
| **8.** | A. kuhamanika | B. kutamauka | C. kuthaminika | D. kudhaminika |
| **9.** | A. kuna | B. pana | C. ina | D. iko |
| **10.** | A. utangamano | B. utengamano | C. utengano | D. utangano |

__11__ baadhi ya wanafunzi hawapendi michezo. Ni muhimu kukumbuka kuwa michezo __12__ manufaa mengi sana kwao. __13__ kwa kweli michezo __14__ watoto __15__ nzuri ya kujifunza mambo mengi.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **11.** | A. Hamkani | B. Maskani | C. Yamkini | D. Makini |
| **12.** | A. zina | B. uno | C. yana | D. ina |
| **13.** | A. Ama | B. Ati | C. Bila | D. Wala |
| **14.** | A. huwapea | B. huwapa | C. hupata | D. huwapasha |
| **15.** | A. fursa | B. wakati | C. ruhusa | D. muda |

© Stepford Press and Publishers, 2021

Jibu swali la 16 mpaka 30, kulingana na maagizo uliyopewa.

16. Chagua sentensi iliyoakifishwa sahihi
   A. "Nitakuja kesho," Dada alisema.
   B. "Utakuja lini?" Mhudumu aliuliza.
   C. "Salaala! Amefunga bao."
   D. "Nitakupa zawadi?" Mwalimu aliahidi.

17. Ni sentensi ipi inayoonyesha wakati uliopita muda si mrefu?
   A. Nimeibuka mshindi na nimepewa tuzo.
   B. Niliibuka mshindi na nikapewa tuzo.
   C. Huibuka mshindi na kupewa tuzo.
   D. Ninaibuka mshindi na ninapewa tuzo.

18. Morio hutembea kwa madaha 'Kwa' imetumika kuonyesha
   A. jinsi
   B. sababu
   C. kifaa
   D. kimilikishi

19. Seremala hutumia __________ kushikia mbao anapozifanyia kazi, naye mwashi hutumia______ kupimia usawa wa ukuta.
   A. timazi, jiriwa
   B. kekee, patasi
   C. filifili, pimamaji
   D. jiriwa, timazi

20. Nyaribari ni nyanyamkuu. Je, atanitaje?
   A. Mjukuu
   B. Kitukuu
   C. Mwana
   D. Kilembwe

21. Neno 'hama' lina maana sawa na
   A. toroka   B. ambata
   C. gura   D. toweka

22. Andika kinyume cha sentensi ifuatayo:
Shaibu alizikwa jana jioni.
   A. Ajuza alizikwa jana jioni.
   B. Shaibu hakuzikwa jana jioni.
   C. Shaibu alizikuliwa jana jioni.
   D. Ajuza hatazikwa jana jioni.

23. Andika ukubwa wa:
Aliumwa na nyuki kinywani mwake.
   A. Waliumwa na nyuki vinywani mwao.
   B. Aliumwa na juki kijinywani mwake.
   C. Yaliumwa na juki kinywani mwake.
   D. Liliumwa na juki jinywani mwake.

24. Nomino '**hekalu**' iko katika ngeli ya
   A. LI - YA
   B. U - ZI
   C. U - I
   D. I - ZI

25. Chagua aina ya pambo ambalo huvaliwa masikioni.
   A. Kipini
   B. Kidani
   C. Kikuba
   D. Mapete

26. Msimu wa mvua nyingi ni__________ ilhali majira ya baridi kali ni __________ .
   A. kifuku, kipupwe
   B. masika, kifuku
   C. mchoo, vuli
   D. kiangazi, kipupwe

27. Chagua kiwakilishi katika sentensi ifuatayo:
Sisi hucheza hadi usiku wa manane wakati wa kibunzi.
   A. hadi
   B. kibunzi
   C. sisi
   D. hucheza

28. Andika wingi wa sentensi ifuatayo:
Ufa ule ukutani una uzi uliofunga waya wa uta.
   A. Nyufa ula ukutani zina nyuzi uliofunga waya wa uta.
   B. Nyufa zile nyutani zina nyuzi zilizofunga nyoya za kutani.
   C. Nyufa zile kutani zina nyuzi zilizofunga nyaya za kuta.
   D. Nyufa zile kutani zina nyuzi zilizofunga nyaya za nyuta.

29. Andika usemi wa taarifa wa kifungu kufuatacho:
"Nitapika biriani kesho," mpishi alisema.
   A. Mpishi alisema kuwa angepika biriani siku iliyofuata.
   B. Mpishi alisema kuwa angepika biriani kesho.
   C. Mpishi alisema kuwa atapika biriani siku iliyofuata.
   D. Mpishi angesema kuwa angepika biriani siku ijayo.

30. Tumia kiunganishi kifaacho zaidi kukamilisha sentesi ifuatayo:
Mwalimu anafundisha darasani __________ wewe unacheza.
   A. lau;
   B. almuradi;
   C. ilhali;
   D. ijapokuwa.

© Stepford Press and Publishers. 2021

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 31 mpaka 40.*

Teknolojia imeleta mfumo mpya wa maisha kote ulimwenguni. Imekuwa **nadra** sana kwa watu wa mataifa kutekeleza kazi zao kivyao. Hii ni kwa sababu mitambo ya tarakilishi imeenea kote na matumizi yake si mapya tena. Hali hii imekuwa msukumo mpya wa maendeleo katika nyanja mbalimbali za nchi kama vile biashara, uvumbuzi wa bidhaa mpya viwandani na vyombo vya **kuonewa fahari** katika makazi ya watu, vikiwemo redio, runinga na majiko.

Kweli, dunia nzima imekuwa kijiji tu hivi, mlango wa kwenu unakabiliana na wa kwetu na mawasiliano, mapatano na uhusiano huo kuwa bayana zaidi. Kale, watu walichukua muda mrefu kuandikiana nyaraka zilizochukua miezi kadhaa kufika; siku hizi huduma hii ya shirika la posta na nyingine hapa na pale si kuzuizi kikubwa kwa mawasiliano na umuhimu wake umeachiwa uwasilishi wa vifurushi. Watu wengi hutuma ujumbe mfupi kwa rununu. Barua pepe nazo ni nyingine ambazo zimeimarisha mawasiliano hasa kutoka mabara; pasi kuwa na gharama kuu kama hapo awali. Kipepesi na mitambo ya umeme vinatumika katika nyanja mbalimbali kote duniani.

Hata hivyo, kila masika yana mbu, nao mbu husambaza malaria. Kupitia vyombo vya habari na mawasiliano, vijana wetu wamechukua hulka za kizungu. Matumizi ya dawa za kulevya, kujivalia nusu uchi na lugha chafu, ni baadhi ya mambo yanayochangia ongezeko la visa vya ubakaji.

Ni kweli kuwa mambo mapya yakija watu hujifunza mengi lakini si yote ambayo huja yana manufaa kwetu.

*© Stepford Press and Publishers. 2021*

**31.** Watu wa mataifa hawawezi kutekeleza shughuli kivyao kwa sababu

A. mawasiliano yamekuwa na gharama kuu.
B. ulimwengu umekuwa kijiji tu.
C. kiwango cha teknolojia kimekuwa sawa kote.
D. mataifa mengine hayana nguvu za umeme.

**32.** Neno **nadra** kama lilivyotumika katika kifungu linamaanisha

A. kawaida
B. muhali
C. mbeleni
D. rahisi

**33.** Ni jambo lipi ambalo limechangia kuunganisha ulimwengu wa sasa?

A. Masomo ya sayansi.
B. Ueneaji wa nguvu za umeme.
C. Uuzaji wa dawa za kulevya
D. Mawasiliano.

**34.** Semi '**kuonewa fahari**' katika kifungu inamaanisha

A. kukejeliwa
B. kuchukiza
C. kujivunia
D. kubezwa

**35.** Barua pepe hutumika nyakati hizi kwa sababu zifuatazo isipokuwa

A. zina gharama ya chini.
B. huchukua muda mfupi kuwasilisha ujumbe
C. uvumbuzi wa teknolojia mpya.
D. watu wote duniani wana elimu ya tarakilishi.

**36.** Shirika la posta na simu ni muhimu hususan katika nyanja za

A. barua za watu.
B. vifurushi.
C. matangazo ya bidhaa.
D. elimu ya mawasiliano.

**37.** Kifaa kitumiwacho kutuma nakala na barua upesi zaidi katika mashirika ni

A. rununu
B. kipepesi
C. tarishi
D. kidubwasha

**38.** Ni methali ipi kati ya hizi inayoeleza kuwa mambo mapya si mabaya kama asemavyo mwandishi?

A. Mgeni njoo mwenyeji apone.
B. Mwacha mila ni mtumwa.
C. Vyote ving'aavyo si dhahabu.
D. Mla nawe hafi nawe ila mzaliwa nawe.

**39.** Kulingana na ufahamu matumizi ya mihadarati yanaongeza visa vya

A. ubakaji
B. wizi
C. usalama
D. mauaji

**40.** Kasoro moja ya teknolojia ni
A. kuwaelimisha watu.
B. kutangaza habari za ulimwengu.
C. watu kupoteza maadili ya kiasili na kuiga ya kigeni.
D. kueneza habari duniani kote.

© *Stepford Press and Publishers, 2021*

*Soma kifungu kifuatacho kisha ujibu maswali 41 mpaka 50.*

Bahati alikuwa amelala kifudifudi kitandani pake, akilia kwi! Kwi! Kwi! Akilia kwa sababu ya majuto, mapenzi na upweke; akililia ndoto zake. Mara alijiona yuko peke yake katika dunia. Ile kamba ya tumaini aliyokuwa akiininginia aliona imeponyoka akawa hana cha kushika. Alijiona hali yuko kwao, tena kitandani pake.

Alisikitika akaona amekimbiwa na mwenyeji wake wa uhai. Sasa hakuthamini kitu chochote kingine ila Idi, ambaye alikwishampoteza. Hakuwa na mwingine, wala asingemtaka mwingine; nani angekuwa kama Idi? Haya ndiyo mawazo aliyokuwa akipigana nayo.

Ah! Lakini aliona yote hayo aliyataka mwenyewe. Yeye ndiye aliyemfukuza, ndiye mkosa na ndiye sababu. Vile alivyofanya sivyo, kabisa sivyo, kwani mapenzi ni kujitolea na kukubali, iwe jema au baya. Lawama zake zilikuwa bure maana yeye ndiye wa kulaumiwa. Alijuta kutumia nguvu; bora angetumia upole na siasa, au angekubali kushiriki jambo aliloambiwa na Idi. Bora ubaya wa nia ya Idi kuliko aliyokuwa nayo sasa. Kwa nini asikubali, kwa nini?

Bahati alilia kwa kite na simanzi, usingizi ukamwonea huruma, ukamchukua hima na kupumzisha kitandani. Alizinduliwa na vishindo vya waenda msikitini, maana tayari kulikwisha pambazuka. Saa ya Bahati siku zote ilikuwa wapita njia. Alikuwa amekwishazoea kukisia wakati kwa miendo ya wale waendao kazini, shuleni, msikitini, ndege za abiria na waadhini.

Punde hivi, alizoazoa juu ya kitanda chake cha mayowe, chenye godoro la usumba, akaketi ukingoni. Macho yalikuwa yameiva na kuvimba, kichwa kikawa kizito, mfano wa mtu aliyekesha. Aliona sakafu ya chumba chake ikienda mrama kama vile chumba hicho kilikuwa kikielea juu ya mawimbi yenye kusukasuka. Bahati alishika hodari kingo za kitanda chake asiporomoke na kuanguka. Kichwani mlikuwa na mgongano wa vipande vya mawazo, kwa sababu ya vituko vya jana.

© Stepford Press and Publishers, 2021

41. Kinyume cha '**kulala kifudifudi**' ni

A. kulala chali
B. kulala kwa ubavu
C. kulala kifundifundi
D. kusinzia

42. Ni kamba gani ya tumaini iliyomponyoka Bahati?

A. Mapenzi na majuto.
B. Mapenzi yake na Idi.
C. Ndoto zake.
D. Alikuwa amebaki pekee duniani

43. Aliyesababisha utengano baina ya Bahati na rafiki yake ni

A. mama yake Bahati.
B. Idi
C. Bahati mwenyewe
D. Fatani

44. Maana ya maneno '**kulia kwa kite na simanzi**' ni

A. kulia kwa sauti na mayowe.
B. kulia bila ya kutoa machozi.
C. kulia kwa uchungu na huzuni.
D. kulia ndani kwa ndani

45. Kulia kwa Bahati kulichachawizwa na

A. wageni
B. usingizi
C. waadhini
D. wapita njia

46. "...... saa ya Bahati siku zote ilikuwa wapita njia." Maana yake ni

A. Bahati aliamshwa na wapita njia.
B. Bahati hakuwa na saa yoyote.
C. Wapita njia walijua saa ya Bahati.
D. Bahati na wapita njia walikuwa na saa moja.

47. Ni ipi kati ya zifuatazo haielezi hali ya Bahati?

A. Mpweke
B. Mwenye hofu
C. Mwenye mawazo
D. Mtulivu

48. Kwa nini Bahati alishika kingo za kitanda chake?

A. Ili asianguke.
B. Ili asiwaze.
C. Ili asione kizunguzungu.
D. Ili aketi.

49. Anayewaita waislamu kwenda kuswali msikitini huitwa

A. Imamu
B. Kadhi
C. Mwadhini
D. Shehe

50. Kamilisha methali ifuatayo:
Mapenzi ni kikohozi
A. hayatambuliki
B. hayafichiki
C. hayaonekani
D. hujulikana

HUU NDIO UKURASA WA MWISHO ULIOPIGWA CHAPA.

© *Stepford Press and Publishers, 2021*